
# 16 Siku za Uanaharakati 2024

## Recommit! Be Accountable! Resource Prevention!

# Mwongozo Wa Shughuli Za Vyombo Vya Habari

Mwongozo huu wa shughuli za vyombo vya habari unatoa mfumo unaoweza kuhamasisha kwa ufanisi Kampeni ya Siku 16 za uhanaharakati za Kukomesha Ukatili wa Kijinsia, kwa kuzingatia umuhimu wa kujitoa tena kupinga ukatili dhidi ya wanawake kupitia mifumo ya uwajibikaji na uhamasishaji wa rasilimali. Inahimiza ushiriki wa vyombo vya aina mbalimbali vya habari, na kuhimiza jukumu la watu binafsi, mashirika na jamii katika kujenga dunia isiyo na ukatili.

## 1. Kampeni ya Mitandao ya Kijamii



Jiunge na mazungumzo katika kanda! Tutatumia majukwaa yetu ya mitandao ya kijamii kama vile, Twitter, Facebook, Instagram, kuungana, kujumuika kwa pamoja ili kukumbatia udada wetu na amali za ufeministi. Wakati wa kampeni, tutashirikishana vibonzo vya Kampeni za Mitandao ambavyo wewe, pia shirika lako mnaweza kusambaza vobonzo hivyo kwenye mitandao yenu. Kumbuka kutumia hashtags zilizo hapo chini kujiunga, tag @GBVNet, na kutangaza jumbe za kampeni kwa watu wengi.

#16Days
#RecommitToBeijing
#TrackThePromise
# Beijing30ActionNow

- Tangaza ahadi za Kampeni: Wahimize watu binafsi kujitoa tena ili kutimiza ajenda za Beijing (k.m. kuzitaka serikali kujitoa tena katika kutetea ongezeko la ufadhili na kutuma ujumbe kwa kutumia hashtags zilizoainishwa hapo juu.
- Jiunge katika vuguvugu hili #16 Days! Shirikisha wengine jinsi unavyojihusisha katika kuzuia/kutokomesha ukatili dhidi ya wanawake. Hebu tujitoe tena kujenga dunia iliyo salama kwa kujenga uwajibikaji na kutoa usaidizi kwa waathirika.

- Shirikisha Watu wenye ushawishi mkubwa: Shirikiana na washawishi wa ndani, wa kanda na wa kimataifa ili kukuza kampeni na kuhamasisha kuchukua hatua. Baadhi ya mapendekezo ya mashirika na taasisi ni pamoja na:
  - Mashirika ya Kimataifa.
    - Ofisi za Nchi za Umoja wa Mataifa
    - Mashirika ya maendeleo ya kimataifa.
    - Mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu yanayofanya kazi za kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake.
    - Taasisi na mifuko ya kimataifa ya haki za wanawake
  - Mashirika ya kanda na mitandao.
    - Mtandao wa Kuzuia UWAKI.
    - Mashirika ya kanda yanazoshughulikia usawa wa kijinsia (k.m. Umoja wa Afrika, jumuiya za kiuchumi za kikanda)
    - Miungano ya haki za wanawake ya kanda na mitandao ya kifeministi.
    - Mashirika ya haki za binadamu ya kanda.
  - Vyombo vya Serikali vya Kitaifa
    - Wizara za Jinsia, Wanawake au Masuala ya Kijamii zenye jukumu la kutekeleza sera za kitaifa za jinsia
    - Wakala wa serikali au idara zilizopewa jukumu la kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.
    - Tume za kitaifa za haki za binadamu .
    - Huduma za kitaifa za msaada wa kisheria au Tume za haki
  - Mashirika ya kutetea haki za Wanawake Katika Nchi.
    - Wanachama wa shirika la Mtandao wa Kuzuia UWAKI
    - Mashirika ya wanawake katika ngazi ya jamii yanayolenga kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na kubadilisha kanuni za kijamii.
    - Mashirika ya kijamii yanayotoa huduma kwa wahanga wa ukatili.
    - Mashirika ya kifeministi yanayotetea mabadiliko ya sera na marekebisho ya sheria.
    - Wizara za Serikali zinazofanya kazi za kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.
  - Taasisi za Taaluma na Utafiti.
    - Chuo kikuu au taasisi za utafiti wa kijinsia zinazofanya tafiti kuhusu kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake.
    - Watafiti wa Kifeministi na mitandao inayoshinikiza mabadiliko ya kijinsia na jitihada za kuzuia ukatili
    - Watu wabobezi waliojikita katika kutetea uwepo wa mifumo madhubuti ya uwajibikaji katika sera za kijinsia.

## 2. Shughuli nyingine za vyombo vya habari.

### Matangazo ya Redio na Runinga.






- Shirikiana na vituo vya redio vya ndani ili kutangaza mahojiano, hadithi za walionusurika na Ukatili, na majadiliano kuhusu umuhimu wa kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.
- Tumia vipindi vya runinga kuangazia huduma za walionusurika na ukatili na kuelezea jinsi jamii inavyoweza kuunga mkono juhudi za kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.
- Andaa vipindi vya matangazo mafupi ya mfululizo kupitia vipindi vya huduma kwa jamii ambayo yanasisitiza ujumbe muhimu wa Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing , ikiwa pamoja na  wito wa kuchukua hatua kwa watu binafsi na mashirika kuazimia upya kukomesha ukatili dhidi ya wanawake. Mifano ni pamoja na:
  - “Katika mwaka wa 1995, Serikali zilitia saini ahadi zilizotokana na Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing ili kuchukua hatua jumuishi za kuzuia na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake. Takribani miaka 30 baadaye, ahadi hizi bado hazijakamilika.”
  - “Ukatili dhidi ya wanawake hauwezi kuendelea bila ya kuchukua hatua. Watunga sera na taasisi za serikali lazima ziazimie upya kukomesha ukatili dhidi ya wanawake kutokana na maono yaliyoainishwa katika Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing.
  - “Kukomesha ukatili kunahitaji utashi wa kuchukua hatua na rasilimali. Kuanzia nyumba salama hadi usaidizi wa kisheria hadi programu zinazobadilisha kanuni kandamizi za kijinsia, serikali lazima zifadhili huduma zinazoendeleza utu na ustawi wa wanawake. Kwa pamoja tunaweza kukomesha ukatili dhidi ya wanawake.”
  - “Paza sauti kudai uwajibikaji kutoka kwa watunga sera na viongozi wa jamii. Kila taarifa inayotolewa ya ukatili dhidi ya wanawake lazima ichukuliwe kwa uzito. Kwa pamoja, tunaweza kujenga jamii salama zaidi!”

## 3. Taarifa kwa Vyombo vya Habari




- Andaa mahojiano na wadau wakuu: viongozi wa jamii, wanaharakati, na wanusurika.
- Angazia malengo muhimu ya kampeni na ujumbe, ukisisitiza mifumo ya uwajibikaji yaliyotolewa kwenye Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing.
- Ainisha sera za kijamii na kitaifa zinazoeleza kwa undani wajibu wa maafisa wa serikali kutekeleza juhudi za kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake.
- Toa taarifa kwenye vyombo vya habari kuhusu hatua muhimu za kampeni, ikiwa ni pamoja na hadithi za mafanikio katika kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

Kuna njia kadhaa za kujihusisha na machapisho! Tumia vyombo vya habari hapo chini kulingana na muktadha wa sehemu uliyopo na ushiriki wa vyombo vya habari vya ndani.

## Taarifa kwa Vyombo vya Habari:
## Kupendekeza kwa mara nyingine kwenye Dira ya Beijing ya Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake - Wito wa Kuchukua Hatua.

Tunapoadhimisha miaka 30 ya Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing, dunia inakabiliwa na wakati muhimu wa kuazimia upya dhamira yake ya kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na wasichana. Kampeni ya Siku 16 za uanaharakati za Kupinga Ukatili wa Kijinsia inatoa wito kwa serikali, mashirika na jamii kusimama kwa pamoja na kuchukua hatua madhubuti kulinda haki za wanawake na kuhakikisha usalama wao.

Katika maadhimisho haya ya kihistoria, tunazihimiza serikali kujitoa tena kwenye ahadi zilizotolewa katika Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing kwa kuunda mifumo thabiti ya uwajibikaji na kutoa ufadhili wa kutosha kwa huduma muhimu za waathirika na programu za kuzuia. Huduma hizi ni pamoja na usaidizi wa kisheria, huduma za afya, nyumba salama, na juhudi za kuzuia zenye misingi ya kanuni za ufeministi, zenye msingi yenye uthibitisho. Ni muhimu kutenga rasilimali muhimu ili kukomesha ukatili unaoendelea kuwaathiri wanawake na wasichana ulimwenguni kote.

Juhudi hizi zinahitaji nia ya dhati na siyo maneno matupu - zinadai kuchukua hatua. Serikali lazima ziimarishe utekelezaji wake wa sheria zinazowalinda wanawake na wasichana dhidi ya ukatili na lazima zianzishe mifumo yenye uwajibikaji na rasilimali ili kuhakikisha ahadi hizi zinatimizwa. Tunatoa wito kwa serikali kutimiza ahadi zao na kujenga dunia ambayo kila mwanamke na msichana anaweza kuishi bila hofu ya ukatili.

Walionusurika wanastahili huduma za kina za usaidizi, ikijumuisha msaada wa kisheria, msaada wa kisaikolojia na upatikanaji wa huduma ya nyumba salama. Huduma hizi lazima ziwe jumuishi na zinazojali tamaduni, zikishughulikia mahitaji ya wanawake wote, wakiwemo wahamiaji, wanawake wenye ulemavu, wasichana wenye umri mdogo, na wanawake walio kwenye makundi maalum. Hakuna mnusurika anayepaswa kuachwa bila ya kupata huduma na ulinzi unaohitaji ili kujenga upya maisha yao na kupata nafuu kutokana na madhara yaliyowapata.

Kukomesha ukatili dhidi ya wanawake kunahitaji mabadiliko ya kimsingi katika mitizamo, tabia na kanuni zinazoshughulikia chanzo cha msingi cha ukatili dhidi ya wanawake: wanaume kuwa na mamlaka dhidi ya wanawake. Tuna wajibu wa kuondoa kanuni kandamizi za kijinsia zinazoendeleza kutokuwepo na usawa na ubaguzi, na kuendeleza mabadiliko ya kijinsia katika viwango vya mtu binafsi, mtu na mtu, na jamii kwa ujumla. Mashirika yanayo tetea haki za wanawake yapewe rasilimali za kutosha na harakati za kuimarisha vuguvugu la kijamii ni za muhimu ikiwa tunatamani kufikia mabadiliko hayo. Mashirika haya, ambayo juhudi zake ni muhimu katika kuimarisha haki za kijinsia, na kuzuia ukatili, yanahitaji ufadhili endelevu na ushirikiano wenye usawa ili kuendeleza kazi zao muhimu.

Tunapoungana kwa pamoja katika Siku 16 za Uanaharakati,tunasimama tukiwa na mshikamano na wanawake wa kila mahali. Tunatoa wito kwa wadau wote - kutoka kwa wafadhili hadi serikali – kujitoa tena kujenga dunia ambayo kila mwanamke na msichana anaweza kuishi bila ukatili. Wakati wa kuchukua hatua ni sasa. Kwa pamoja tunaweza kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na wasichana.

Raising Voices

16 DAYS

GBV PREVENTION NETWORK

Building Momentum•Fostering Activism